**OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MTAA**
**MKOA WA IRINGA**
**MWONGOZO WA USAHIHISHAJI**
**MTIHANI WA UTAMILIFU KISWAHILI KIDATO CHA NNE**
**MAY 2023**

1. Alama 10

| i | Ii | iii | iv | v | Vi | vii | viii | ix | x |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | D | B | D | B | D | D | A | A | E |

2. Alama 06

| I | ii | iii | Iv | v | vi |
|---|---|---|---|---|---|
| E | A | F | B | D | C |

3. Alama 09
   Mwanafunzi anatakiwa abainishe hoja(alama0.5) Pamoja na mfano mmoja(alama 0.5).
   i. Utohoaji mfano, Bunge
   ii. Urudufishaji mfano, Polepole
   iii. Uambatanishaji mfano, Mwananchi
   iv. Kufananisha sauti mfano, Pikipiki
   v. Ufupishaji mfano, UKIMWI
   vi. Uambishaji mfano, wanalima
   vii. Unyambulishaji mfano chezea
   viii. Kubadili fonimu/sauti mfano Lima, Lami, Imla n.k
   ix. Kuangalia kazi ya kitu mfano Kipima pembe
4. Alama 09
   A) Viambishi awali ni mofimu ambazo hupachikwa kabla ya mzizi wa neno. (alama 03)

   B) i) Nafsi mfano **A**nakula
   ii) Urejeshi mfano Nili**ye**mpiga
   iii) Ukanushi mfano **Ha**kulima
   iv) Masharti mfano A**ki**ja (alama 03)

   C) i) **ye/o** mfano Ali**ye**pewa na Wali**o**pewa
   ii) **o/yo** mfano Uli**o**katika na Ili**yo**katika
   iii) **-ko**- mfano kuli**ko**bomoka
   iv) **PO/MO/KO** Pali**po**, Wali**mo** na kuli**ko** **(alama 03)**
5. Alama 09
   A) Mtahainiwa aeleze chanzo cha lahaja na umuhimu wake katika lugha.
   Chanzo cha lahaja
   i) Utengano wa kiijografia
   ii) Matabaka ndani ya jamii

www.WazaElimu.com

iii) Kupita kwa wakati
iv) Mwingiliano wa kijamii katika ndoa na shughuli zingine
v) Kuhama hama kwa watu (alama 04)

Umuhimu wa lahaja
i) Kukuza lugha
ii) Kusanifisha lugha
iii) Kupamba lugha
iv) Kutuonesha mitindo mbalimbali ya uzungumzaji
v) Kukamilisha mawasiliano (alama 05)

6. TATAKI Taasisi ya taaluma za Kiswahili. Ilianza mwaka 2009, ilibadiliswa jina kutoka TUKI mpaka TATAKI.
Malengo ya TATAKI (alama 03)
i) Kutafsiri maandishi yafaayo katika Kiswahili
ii) Kufanya utafiti, kuiendeleza na kuikuza lugha ya Kiswahili katika Nyanja zake zote(isimu, fasihi na utamaduni wa Kiswahili)
iii) Kufundisha taaluma mbalimbali za Kiswahili.
iv) Kuratibu msamiati na kuunda istilahi anuahi za kitaaluma na kuziingiza katika kamusi.
v) Kushirikiana na taasisi Pamoja na asasi nyingine za kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili.

Mafanikio ya TATAKI (alama 03)
i) Taasisi imeweza kudahili na kufundisha wanafunzi wa shahada za awali, umahili na uzamivu.
ii) Taasisi imefanikiwa kusimamia na kufundisha lugha ya Kiswahili kwa wageni.
iii) Taasisi imefanya tafiti mbalimbal;I kuhusu lugha ya Kiswahili na kuchapisha matokeo ya tafiti hizo katika vitabu na majarida.
iv) Taasisi imefanikiwa kuendelea kuboresha kamusi mbalimbali zilizotolewa hapo awali mfano, KAMUSI YA KISWAHILI SANIFU na KAMUSI YA KISWAHILI-KINGEREZA
v) Taasisi imeandaa semina, warsha na makongamano ya ndani na ya kimataifa

Changamoto za TATAKI (alama 03)
i) Uhaba wa vifaa vya kisasa vinavyoendana na kasi ya mabadiliko ya sayansi na teknolojia kama vile vifaa maalumu vya ukalimani na maabara ya lugha.
ii) Baadhi ya wataalamu kuacha kufanya kazi za Kiswahili na kujihusisha na kazi nyingine.( Uhaba wa wataaalamu)
iii) Taasisi hupata fedha kidogo ambazo hazikidhi maitaji ya kujiendesha kwa ufanisi(Uhaba wa fedha)

7. Mwanafunzi aeleze chanzo na namna ya kuondoa utata katika lugha.
Chanzo cha utata (alama 05)
i) Neno kuwa na maana zaidi ya moja
ii) Kutokuzingatia mazingira au muktadha wa wazungumzaji.
iii) Matumizi ya lugha ya picha
iv) Matumizi ya kauli ya kutendeka

v) Mtumiaji wa lugha kukosa ala fulani au kitheme.

Namna ya kuondoa utata (alama 04)

i) Kufafanua maneno yenye tungo zenye maana zaidi ya moja
ii) Kutumia maneno kwa kuzingatia mazingira au muktadha wa wazungumzaji
iii) Kuzingatia matumizi sahihi za alama za uandishi katika tungo.
iv) Kuzingatia upatanisho wa kisarufi mfano Nimenunua Mbuzi wawili sio nimenunua mbuzi mbili

8. A) Mtahiniwa aandike barua ya kikazi ya kibiashara ya kuomba kuagiziwa zana za kilimo
Mambo ya msingi anayotakiwa kuzingatia katika barua yake

i) Anuani ya mwandishi
ii) Tarehe
iii) Anuani ya mwandikiwa
iv) Salamu za awali
v) Kichwa cha barua
vi) Mwanzo wa barua
vii) Kiini cha barua(orodha ya bidhaa husika na gharama zake)
viii) Mwisho wa barua
ix) Sahihi na jina
x) Cheo cha mwandishi

B) i) Ua si ruwaza njema, tuzo ya mtu kupewa (alama 01)
ii) ''wa'' (alama 01)
iii) Mtindo wa kimapokeo kwasababu shairi limefuata urari wa vina na mizani. (alama 01)
iv) Muundo ni tarbiha kwa sababu shairi limejengwa kwa mistari minne kwa kila ubeti. (alama 01)

**NB: Na majibu mengine yanayofanana na hayo**

9. Mtahiniwa aelezee mambo yanayo elimisha na vutabu vya mashairi kama vile
WASAKATONGE

i) Kupiga vita rushwa katika shairi la KANSA
ii) Kukemea vitendo vya tohara kwa wanawake katika shairi la TOHARA
iii) Kukemea vitendo vya usagaji au mapenzi ya jinsia moja katika shairi la JIWE SI MCHI (alama 06)

MASHAIRI YA CHEKACHEKA

i) Kukemea vitendo vya rushwa katika shairi la MWINYI UMEWASHA MOTO
ii) Kukemea vitendo vya uongozi mbaya katika shairi la CHURA UMEGUNDULIKA
iii) Kukemea vitendo vya matumizi mabaya ya fedha za umma katika shairi la GUNIA LA MIKUTANO (alama 06)

MALENGA WAPYA

I) Kupiga vita matabaka katika shairi PUNDA
II) Kupiga vita uongozi mbaya katika shairi la PUUZO
III) Kupiga vita unyonyaji katika shairi la SAMAKI MTUNGONI (alama 06)

**Utangulizi alama 02 na hitimisho alama 01**

**10.** Mtahiniwa afafanue maana ya fani (alama 02)

Kiini, Mtahiniwa aeleze vipengele vya fani jinsi vilivyokamilisha kazi za waandishi wawili wa vitabu vya riwaya.

JOKA LA MDIMU

**i)** Mandhari, kama vile Ofisini, Mbuga za Wanyama na nyumbani.
**ii)** Mtindo, Masimulizi na Mtindo wa nafsi ya tatu umoja
**iii)** Wahusika, kama vile BROWN KWACHA
**iv)** Matumizi ya lugha, lugha ni nyepesi na yenye kueleweka vizuri

WATOTO WA MAMA NTILIE

i) Wahusika mfano Mzee Lomolomo kuelezea vitendo vya ulevi
ii) Mandhari, Mandhari ya nyumbani na vilabuni
iii) Mtindo, Mtindo wa masimulizi na Wimbo

TAKADINI

i) Mandhari, Mandhari ya Nyumbani, Polini na Mtoni
ii) Wahusika mfano Takadini, Sekai
iii) Mtindo, Mtindo wa masimulizi na nyimbo

11. Utangulizi; maana ya Wahusika (alama 1.5)

Mtahiniwa awafafanue Wahusika wenye matendo yanayochukiza jamii kama vile

ORODHA

i) Furaha-Mtoro, Awasikilizi wazazi, Aliingia kwenye makundi mabaya, mzinzi n.k
ii) Ecko-Malaya, Msaliti,
iii) Padre Jamesi- Msaliti, Mzinzi, Anakiuka maagizo ya kanisa lake

KILIO CHETU

i) Chausiku-Anatembea na Watoto wadogo, Malaya
ii) Joti-Anajiunga na makundi mabaya, Anaangalia picha za uchi
iii) Suzi-Mtumiaji wa dawa za uzazi wa mpango

NGOSWE PENZI KITOVU CHA UZEMBE

i) Ngoswe-Kuchanganya mapenzi na Kazi n.k
ii) Mazoea- Usaliti
iii) Mitomingi- Mlevi, Mvivu

www.WazaElimu.com